



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA MWANZA



SHERIA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA
NAMBA 5/2019 KIFUNGU CHA 21 (a-I)

UWEZO NA HAKI ZA MAMLAKA.

- Kujenga na kusimamia miundo mbinu ya maji.
- Kupewa njia kwa ajili ya kulaza mabomba ya kusambaza Maji
- Kufunga mita za kupima matumizi ya maji ya wateja.
- Kutoza Ankara kwa huduma ya majisafi na majitaka.
- Kuingia mkataba na mtu mwenye eneo la ardhi kwa ajili ya kulitumia kuboresha utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira.
- Kuweka masharti ya matumizi ya huduma ya maji kutokana na sababu maalum.
- Kutoa vifaa kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya huduma ya majisafi na majitaka
- Kuingia mikataba ya kibiashara kwa lengo la kupokea majitaka kwenye mfumo wa majitaka.
- Kuzuia utupaji wa taka zisizoruhusiwa kwenye mfumo wa majitaka.
- Kuingia katika makazi yeyote yenye huduma na kufanya shughuli inayohusiana na huduma ya maji na usafi wa mazingira.

■Kutunga sheria ndogo kwa lengo la kuwezesha ufanisi wa utekelezaji wa sheria mama namba 5/2019

■Kuzalisha na kuuza maji ya jumla kwa wauzaji wadogo wadogo.

KAZI NA WAJIBU WA MAMLAKA:
Kifungu 20(a-I)

- Kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa mujibu wa sheria.
- Kuhakikisha upatikanaji wa huduma inayokidhi viwango vya ubora.
- Kuendeleza na kulinda miundo mbinu ya maji na usafi wa mazingira.
- Kutunza vyanzo vya maji kwa kushirikiana na vyombo vingine.
- Kuishauri Serikali kuhusu sera na miongozo kuhusu viwango vya ubora wa huduma.
- Kupanga na kutekeleza miradi mipya ya maji na usafi wa mazingira.
- Kuelimisha umma kuhusu uhusiano wa afya ya jamii na huduma za maji na usafi wa mazingira.
- Kuboresha huduma kwa kushirikiana na vyombo vingine vya serikali.
- Kutoza na kukusanya Ankara na ushuru wa huduma.
- Kufanya tiba ya maji na majitaka kwa viwango vilivyowekwa